
JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAJI

# MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MJINI DODOMA (DUWASA)




## TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MRADI WA MAJISAFI NZUGUNI

Imeandaliwa na: -
Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,
DUWASA,
S.L.P 431,
Email: md@duwasa.go.tz
Website: www.duwasa.go.tz
Simu: +255 26 2324245
Fax: +255 26 2320060

**DODOMA** **April 2024**

# TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MRADI YA MAJISAFI NZUGUNI PHASE I

## 1 Mradi wa Nzuguni Phase I

### 1.1 Lengo la Mradi

Kuboresha huduma ya usambazaji Maji katika Mji wa Dodoma kwa kuongeza uzalishaji wa maji kutoka lita **68,600,000** hadi **76,000,000** kwa siku, sawa na ongezeko la asilimia **11.7** kwa siku.

### 1.2 Hatua za Utekelezaji

Mpaka sasa mradi umefikia **asilimia 96%.** DUWASA inatekeleza ujenzi wa mradi huu kwa kutumia wazabuni saba (7) ambao ni; ***Tanesco, Tanelec Limited Arusha, Master Drilling and Exploration Ltd***, ***Help Desk Ltd**, **Davis & Shitriff Ltd, Judex Contractors na Tanzania Steel Pipes*****.** Kazi zinazofanyika ni pamoja na uchimbaji na uendelezaji wa visima vinne (04), ununuzi wa *transformer* sita, ujenzi wa mtandao wa kusafirisha na kusambaza maji wenye takribani **kilomita 7**, ujenzi wa matenki mawili yenye jumla ya ujazo wa lita **3,500,000**, ujezi wa vibanda vya kuendeshea pampu, ujenzi wa ofisi ya mradi, usimikaji wa pampu za kusukuma maji, ujenzi wa miundombinu ya umeme, ujenzi wa *fire hydrants,* upandaji wa miti, pamoja na ufungaji mfumo wa kompyuta wa ***SCADA*** utakaofanya mfumo huu uweze kujiendesha wenyewe. Mradi upo hatua ya mwisho wa umaliziaji wa kazi ndogondogo(*snags*) kama ujenzi wa fensi kwenye majengo na matenki, ujenzi wa mnara wa kuwekea mfumo wa kutibu maji (*chroline dosing tower*) pamoja na marekebisho madogomadogo.

### 1.3 Gharama za Mradi

Mradi huu una jumla ya mikataba **saba (7)** yenye thamani ya **Tsh. 4,391,901,658.77** Fedha zote za kutekeleza mradi huu zinatolewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia mapato yake ya ndani. Hadi sasa kiasi cha **Tsh. 3,101,221,461.56** kimelipwa kwa wakandarasi wote, sawa na **asilimia 71.**

### 1.4 Muda wa mradi

Mradi huu unatekelezwa kwa kipindi cha miezi sita kutoka tarehe ya kusaini mkataba na kupokea malipo ya awali. Mradi ulianza tarehe **7/2/2023** na ulitegemea kukamilika tarehe **7/8/2023,** lakini kutokana na changamoto ya kuchelewa kwa malipo ya awali pamoja na kazi za nyongeza, mradi unatarajiwa kukamilika tarehe **15/01/2024**

### 1.5 Faida/Mafanikio ya Mradi

Mradi huu unalenga kuhudumia watu wapatao **75,968** katika eneo la **Nzuguni, na baadhi ya maeneo jirani ya Kisasa, Ilazo na Swaswa.** Baada ya kukamilika kwa mradi huu uzalishaji wa maji utaongezeka kutoka wastani wa **50%** hadi **61.7%** ya mahitaji kwa siku.

### 1.6 Changamoto za Mradi

Kutokuendelea kwa kazi kutokana na malipo ya wakandarasi kuchelewa. Mpaka sasa wakandarasi wanadai hati za malipo zenye jumla ya **Tsh. 1,938,013,594.88** kama inalivyochanganuliwa hapa chini.

| No. | Jina la Mkataba | Mzabuni/ Mkandarasi | Gharama za Mkataba (Tsh.) | Kiasi Kilichopokelewa (Tsh.) | Kiasi kilicholipwa (Tsh.) | Kiasi Kilichobaki (Tsh.) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | *Supply and Installation of 500m3 and 3000m3 Galvanized Steel Water Tanks, to be used as Sump and Storage Tank at Nzuguni Water Project-Dodoma* | Helpdesk Engineering Tanzania Limited | 1,739,552,272.94 | 521,865,681.88 | **971,865,681.88** | 1,217,686,591.06 |
| 2 | *Supply of Steel Pipes and Fittings for Nzuguni Water Project-Dodoma* | Tanzania Steel Pipes Limited | 1,164,844,943.95 | 1,026,399,967.23 | 1,026,399,967.23 | 138,444,976.72 |
| 3 | *Supply and Installation of Submersible Pumps, Chlorine Dosing and SCADA System for Automatic Operation for Nzuguni Water Project - Dodoma* | Davis &Shirtliff (T) Limited | 696,777,481.28 | 487,744,236.89 | 487,744,236.89 | 209,033,244.39 |
| 4 | *Construction of Water Supply project at Nzuguni Area.* | Judex Contractors Limited | 477,986,000 | 105,137,217.29 | **297,206,560.00** | 372,848,782.71 |
| 5 | *Supply of Transformers* | Tanelec Limited Arusha | 93,225,560.00 | 93,225,560.00 | 93,225,560.00 | - |
| 6 | *Drilling of 5 Boreholes at Nzuguni* | Master Drilling | 219,515,400.60 | 219,515,400.60 | 219,515,400.60 | - |
| 7 | *Connection of Electricity to Nzuguni* | Tanesco | 5,264,054.96 | 5,264,054.96 | 5,264,054.96 | - |
| | **Jumla** | | **4,397,165,713.73** | **2,459,152,118.85** | **3,101,221,461.56** | **1,938,013,594.88** |

## 2 HITIMISHO

DUWASA inaishukuru Serikali ya awamu ya **Sita (6)** kupitia Wizara ya Maji kwa kuendelea kuipa kipaumbele Dodoma hususani DUWASA katika kutatua changamoto za upatikanaji wa maji Mjini Dodoma.